# 1. Misingi ya viuawadudu

## Mada ya 1e

# Hatari ya viuawadudu

# JARIDA LA UHAKIKA

## 1. Misingi ya viuawadudu

## <u>**Mada ya 1e:**</u> Hatari ya viuawadudu

Viuawadudu ni salama kama vitatumiwa kulingana na kibandiko cha maelezo na watu walio na uzoefu na wanaojua jinsi ya kuchukua tahadhari. Tahadhari italingana na kiwango cha hatari. Kama kiuawadudu ni sumu sana, tahadhari nyingi zitafaa kuchukuliwa kushinda kama kina kiwango cha chini cha sumu. Sheria ni kuwa, shughulikia viuawadudu vyote na uangalifu mkubwa na tahadhari, kwa sababu husababisha madhara makubwa kwa binadamu na mazingira.

**Viuawadudu na mwili wa binadamu**
Mwili wa binadamu ndio huathiriwa kwanza kunapokuwa na matumizi mabaya ya viuawadudu. Viuawadudu vinaweza kuingia mwilini kupitia njia tatu:

- Ngozi: Kupitia ngozini (ngozi na macho).
- Kumezwa: Kupitia mdomoni.
- Mapafuni/kupumuliwa: kupitia kupumua (kuvutwa hadi mapafuni).

Hatari ifuatayo inaweza kutokea kwa mwili wa binadamu:

| Njia ya kuingia mwilini | Sababu ya kuchafuliwa | Njia ya kuzuia |
|---|---|---|
| **Ngozi** | • Kutovaa kinga inayofaa.<br>• Kunyunyiza viuawadudu kukiwepo upepo.<br>• Ajali wakati wa kuchanganya.<br>• Kuto osha mikono baada ya kushughulikia viuawadudu.<br>• Kuvaa nguo zilizochafuliwa. | • Soma kibandiko cha maelezo.<br>• Vaa mavazi ya kujikinga.<br>• Kuwa muangalifu unapotumia viuawadudu.<br>• Osha mikono baada ya kushughulikia viuawadudu.<br>• Anza kila siku na nguo mpya na mavazi ya kujikinga |
| **Mdomoni** | • Kuhifadhi viuawadudu katika chupa za vinywaji na chakula.<br>• Kula, kunywa, au kuvuta sigara unaposhughulikia viuawadudu.<br>• Kutokinga mdomo unaposhughulikia viuawadudu. | • Soma kibandiko cha maelezo.<br>• Usitumie tena vyombo vitupu.<br>• Usile, kunywa wala kuvuta sigara unaposhughulikia viuawadudu, osha mikono vizuri kabla ya kufanya hivyo.<br>• Tumia mavazi ya kujikinga kwa wakati wote unaposhughulikia viuawadudu. |
| **Kupitia** | • Kutovaa kinga inayofaa. | • Soma kibandiko cha maelezo. |

| | | |
|---|---|---|
| **mapafuni/kupumuliwa** | • Kushughulikia miundo ya viuawadudu ya poda bila uangalifu unaofaa.<br>• Unaposhughulikia kemikali fukivu katika maeneo yaliofungwa. | • Tumia mavazi ya kujikinga kwa wakati wote unaposhughulikia viuawadudu.<br>• Shughulikia kemikali fukivu katika maeneo yanayopisha hewa safi na utumie mavazi ya kujikinga sahihi. |

Madhara/matokeo ya uchafuzi wa kila sehemu ya mwili yameelezwa kwa kina katika mada ya 26a kuhusu ni kwa nini mavazi ya kujikinga ni muhimu.

**Viuawadudu na mazingira**
Kila kitu kinachotuzunguka ni mazingira, pamoja na wanyama. Sehemu au maeneo fulani ya mazingira ni rahisi kuathirika na uchafuzi wa viuawadudu kuliko mengine:

- Visima, vidimbwi, maziwa, mito, na maji ya chini ya ardhi.
- Mashamba yaliolimwa na yana mimea ya mazao.
- Mashamba ambayo hayajalimwa na yana mimea mwitu na wanyama wa porini.

Hatari zifuatazo zinaweza kutokea kwa mazingira

| Eneo | Sababu za uchafuzi | Madhara ya uchafuzi | Njia za kuzuia |
|---|---|---|---|
| Vyanzo vya maji | • Kutupa vyombo vitupu kwa njia isio sahihi.<br>• Kutupa bila uangalifu mabaki ya michanganyiko ya viuawadudu.<br>• Vyombo vinavyovuja au kumwaga viuawadudu.<br>• Kuelekea kando kwa kiuawadudu kinaponyunyizwa. | Maji iliochafuliwa ambayo yaweza:<br>• Yatawafanya wanyama na watu kuwa wagonjwa baada ya kunywa au kutumia maji hayo.<br>• Kudhuru samaki au mimea majini. | • Soma kibandiko cha maelezo.<br>• Tupa vyombo vitupu na mabaki mbali na vyanzo vya maji.<br>• Shughulikia viuawadudu vilivyomwagika na ajali mara moja.<br>• Usinyunyize viuawadudu kama kuna upepo mkali. |
| Mashamba yaliolimwa na yana mimea ya mazao. | • Kuchanganya viuawadudu kolevu/enye nguvu kushinda ilivyoagizwa.<br>• Kunyunyiza kiuawadudu kupita kiasi. | • Kuharibu mazao. | • Soma kibandiko cha maelezo.<br>• Changanya na kutumia viuawadudu kulingana na maagizo. |
| Mashamba ambayo | • Kutupa vyombo vitupu kwa njia isio | • Kuharibu mimea.<br>• Kufanya | • Soma kibandiko cha maelezo. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| hayajalimwa na yana mimea mwitu na wanyama wa porini. | sahihi.<br>• Kutupa bila uangalifu mabaki ya michanganyiko ya viuawadudu.<br>• Vyombo vinavyovuja au kumwaga viuawadudu.<br>• Kuelekea kando kwa kiuawadudu kinaponyunyizwa. | wanyama wawe wagonjwa. | • Tupa vyombo vitupu na mabaki mbali na vyanzo vya maji.<br>• Shughulikia viuawadudu vilivyomwagika na ajali mara moja.<br>• Usinyunyize viuawadudu kama kuna upepo mkali. |

# MWONGOZO

## 1. Misingi ya viuawadudu

## <u>Mada ya 1e:</u> Hatari ya viuawadudu

### Vifaa vinavyohitajika:

☑ Ubao ulio na makaratasi

☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)

### Muda unaohitajika: Dakiki 30

### Maandalizi:

☑ Makaratasi ya kufungua kurasa yalio na kichwa: *Hatari ya viuawadudu*

## Mwanzo

| | |
|---|---|
| **U**sikivu: | Waambie washiriki kwamba viuawadudu vyaweza kuwa muhimu sana lakini pia hatari sana. |
| **K**ichwa: | Waambie kichwa: *Hatari ya viuawadudu.* |
| **K**usadikika: | Elezea uzoefu wako katika matumizi bora ya viuawadudu. |
| **M**alengo: | Kuelezea aina tofauti za hatari zinazosababishwa na viuawadudu kwa binadamu na mazingira. |
| **M**anufaa: | Kujua aina tofauti za hatari zinazosababishwa na viuawadudu kutakusaidia kuelezea wateja wako walio wakulima hatari ilioko na tahadhari zinazofaa. |
| **M**welekeo: | Katika kipindi hiki, tutaangazia aina za hatari zinazosababishwa na viuawadudu. Hatutajadili mavazi/vifaa vya kujikinga au huduma ya kwanza iwapo usumishaji. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Waambie washiriki kwamba viuawadudu ni salama kama vitatumiwa kulingana na kibandiko cha maelezo na watu walio na uzoefu na wanaojua jinsi ya kuchukua tahadhari. Kwa upande mwingine, viuawadudu vinaweza kusababisha **madhara makuu na uharibifu** kwa binadamu na mazingira kama havitashughulikiwa kwa uangalifu na bila kuchukua tahadhari.
2. Waambie washiriki kwamba tutaanza na **binadamu.** Uliza kama wanajua vile viuawadudu vinaweza kuingia mwilini. Vinaweza kuingia kutumia njia tatu: **ngozi** (ngozi na macho), **kumezwa** (mdomo), na **kuvutwa mapafuni** (kupumuliwa).
3. Waulize **vile** hii inaweza kufanyika. Hii inaweza kufanyika kama watu hawavai mavazi/vifaa vya kujikinga; wanavaa mavazi/vifaa vilivyochafuliwa; kunyunyiza viuawadudu kama kuna upepo mkali; kupata ajali unapochanganya; kutojiosha baada ya kutumia viuawadudu; kutumia tena vyombo vitupu; kula au kunywa wakati unaposhughulikia viuawadudu; kufanya kazi katika maeneo yaliofungwa; n.k. Andika majibu yote kwa karatasi katika maneno makuu.
4. Uliza washiriki jinsi ya **kuepuka kuchafuliwa**. Tunaweza kuepuka kuchafuliwa kwa kusoma kibandiko cha maelezo; kutumia mavazi ya kujikinga; kuosha baada ya matumizi; kuosha vifaa/mavazi ya kujikinga baada ya matumizi; kutumia kwa njia bora; kutotumia tena vyombo vitupu; kutokula, kutokunywa wala kuvuta sigara unaposhughulikia viuawadudu; n.k; n.k. Andika majibu yote kwa karatasi katika maneno makuu.
5. Waambie kwamba katika kipindi kingine tutajadili kwa kina **madhara/matokeo** ya uchafuzi kwa binadamu na vile tunaweza kujikinga na vifaa/mavazi ya kujikinga.
6. Endelea na mazingira. Waambie kwamba tutaangazia vyanzo vya maji, mashamba yaliolima yalio na mimea, mashamba ambayo hayajalimwa na yana mimea na wanyama. Waulize vile maji, mazao, na mimea na wanyama vinavyoweza kuchafuliwa. Hii inaweza kufanyika kutokana na utupaji usio sahihi wa vyombo vitupu; utupaji bila uangalifu wa mabaki ya michanganyiko ya viuawadudu; vyombo vinavyovuja na kumwagika; kwenda kando kwa kiuawadudu kinaponyunyizwa; n.k. Andika majibu yote kwa karatasi katika maneno makuu.
7. Uliza **madhara/matokeo**. Yanaweza kuwa uchafuzi wa maji; kuharibu mazao; kuharibu mimea; kufanya binadamu, samaki, na wanyama kuwa wagonjwa; n.k. Andika majibu yote kwa karatasi katika maneno makuu.
8. Uliza unavyoweza kuepuka kuchafua mazingira. Tunaweza kuepuka kuchafua kwa kusoma kibandiko cha maelezo, kusuuza mara tatu, kutupa vyombo vitupu inavyofaa, kushughulikia kuvuja na kumwagika kwa viuawadudu mara moja, kuchanganya na kutumia viuawadudu kufuatana na maagizo; kutupa vyombo vitupu na mabaki ya michanganyiko mbali na vyanzo vya maji; n.k. Andika majibu yote kwa karatasi katika maneno makuu

# Malizia

**M**uhtasari: Peana muhtasari kwa kuwaambia kwamba, kama havitashughulikiwa vizuri, viuawadudu vinaweza kuingia mwilini kupitia ngozi, mdomo, na kuvutwa/kupumuliwa. Viuawadudu pia vinaweza kuharibu vyanzo vya maji na mazingira kama havitatumiwa kwa uangalifu.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Waulize vile viuawadudu vinaweza kuingia mwilini. Waulize vile vinaweza kuharibu mazingira na uwaulize tunachoweza kufanya ili kuzuia uharibifu kwa mazingira unaotokana na viuawadudu.

**H**atua fuatilizi: Katika kipindi hiki, tulijifunza kuhusu aina ya hatari zinazosababishwa na viuawadudu. Katika vipindi vingine, tutajadili madhara ya uchafuzi wa binadamu, mavazi/vifaa vya kujikinga, na huduma ya kwanza.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.